


# UHAI

 Waangalie tu hawa jamaa wadogo. Jamani, jamani! Mavuno ya kesho. Mnajua, nafikiri labda sisi sote ni kundi la kawaida la maskani hapa. Lakini ikiwa, kwa bahati, kungekuwako na mtu fulani hapa, ambao ndiyo mara yao ya kwanza kuwa pamoja nasi, bila shaka tunataka kuwakaribisheni. Nasi tunataka kuweka wazi jinsi ambavyo tunawaweka wakfu watoto kwa Bwana.

<sup>2</sup> Mnaona, katika Biblia, mara nyingi tuna watu siku hizi, ambao hufanya maamuzi ya jinsi wanavyopaswa kufanya mambo haya. Lakini sisi tu, hapa, tunajaribu kudumu moja kwa moja na jinsi hili Neno la kale lililobarikiwa linavyofanya jambo hilo. Kisha, na kamwe halizeeki, daima ni mpya kwa sababu ndiyo njia ya Mungu ya kufanya mambo.

<sup>3</sup> Sasa wakati Mwokozi wetu aliyebarikiwa alipokuwa hapa, Bwana Yesu, walipomletea watoto wadogo afanye hiyo kazi, ama heshima inayopaswa kupewa watoto wadogo, mbona, Yeye aliwachukua mikononi Mwake na kuwabariki. Naye akasema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu, kwa maana walio kama hao Ufalme wa Mbinguni ni wao.”

<sup>4</sup> Nao wakawaleta watoto wadogo, na kuwaweka wakfu. Kwa maneno mengine, waliwakabidhi Kwake tu, Naye akawabariki. Na sasa tumeachiwa, kama Kanisa, kuiendeleza kazi aliyofanya alipokuwa hapa duniani. Na hivyo ndivyo tunajaribu kufanya.

<sup>5</sup> Na hakika tuna kundi la watoto wadogo wazuri wamelala kifuani mwa baba zao, asubuhi ya leo. Na ninii tu. . . Jamaa mdogo wa Ndugu Junior. Na Junie, Junie mwingine hapa, mtoto wa Weber. Na—na mtoto wa Ndugu Stricker. . . Hebu tuone, naamini huyu ni msichana; msichana, na mvulana. Wasichana wawili na mvulana. Sawa. Hilo ni sawa. Na yule mtoto pale, ulikuwa naye, au alikuja tu pamoja nawe. Hilo ni sawa.

<sup>6</sup> Vema, nina shukrani na furaha kwamba Bwana ameyabariki makazi yenu kwa zawadi hizi za ishara hizi ndogo za upendo. Unajua, inapofikia mahali ambapo—ambapo wanawake hawawapendi watoto, tena, wao si wanawake tena, nionavyo mimi. Nawapenda jamaa wadogo, na—na—na kitu fulani kuwahusu.

<sup>7</sup> Jamaa wangu mdogo huko nyuma, yeye ni. . . Meda alisema, “Ulikuwa mzee sana kumpata huyo.”

<sup>8</sup> Nikasema, “La, Mungu anapowatuma, wako tu kwa wakati mzuri. Hiyo ni kweli. Wako kwa wakati mzuri hasa. Na kwa hivyo najua inavyoamaanisha, kwa nyumba.

<sup>9</sup> Na vijana wengi, wanasema, “Vema, hatuwezi kupata watoto. Tutangojea mpaka tuwapate baadaye kidogo, na kadhalika.” Jinsi tu Mungu anavyowatuma, wapokeeni, kwa sababu wao ndio kifungo kinachoifunganisha mioyo na nyumba pamoja, watoto wadogo.

<sup>10</sup> Sasa, tutashuka pamoja na wazee hapa, tafadhali, kwa jamaa huyu mdogo hapa, kwa kuwa yuko mkono wetu wa kulia, tukihakikisha. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>11</sup> Mimi pamoja na mke wangu, huko nyuma, tulikutafuta Arizona, majuma machache yaliyopita, kule Parker, kila mahali, tukijaribu kujua uliko, tukashindwa. Nao wananiambia ulikuwa huko kwenye risavu ng’ambo ya mto, huko, kwa hiyo nilikukosa. Na nilisikia mkeo alikuwa mgonjwa, ndipo nikamwambia Ndugu Hooper akwambie umlete hapa ili tuombe pamoja naye. Tutawaombea wagonjwa, ninii. . . isipokuwa awe ni mgonjwa sana, sana na anataka kuombewa sasa.

<sup>12</sup> Tutafanyiza m—mstari katika muda kidogo tu, mara nikizungumza kidogo. Au, je, ulikusudia nizungumze, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, “Naam, bwana.”—Mh.]

<sup>13</sup> Tangazo moja ninalotaka kufanya, asubuhi ya leo. Halafu, basi, hatutazungumza kwa muda mrefu, kisha labda tuumalieze usiku wa leo. Kulikuwa na tangazo hili, ambalo tunatamani. . . Ikiwa mtu yeyote anaishi katika ujirani huu, kwamba wahakikishe kuzungumza na majirani kuhusu suala hili. Majirani wamekuwa wakinipigia simu hapa. Hasa mmoja, katika ujirani, alinipigia simu juzi, na ilihusu wavulana kucheza mpira kwenye hii ploti hapa. Walikuwa na dirisha lililovunjika, mlango wa skrini uliopondeka, bustani iliyovunjika. Kasema. . . Hao jamaa wadogo, majirani wote wanajua wanataka kucheza. Hakika. Wao ni watoto tu. Lakini walirusha mpira wao ukavuka kote na—na kuzivunja bustani zao na kadhalika. Nami nafikiri kuna wavulana kadhaa hapa, katika ujirani, wamejumuishwa.

<sup>14</sup> Nao—nao wamekuwa wema sana kwetu. Hawajawahi kulalamika, majirani, usiku. Nasi tunapiga kelele kidogo hapa, mwajua, usiku sana, lakini hawanung’ini. Nanyi mnajua jinsi wangeweza; wangeweza kutugombanishia hilo, kama wangelitaka. Nasi tunaamini kudumisha amani kabisa na majirani zetu, na pamoja na. . . “Ishi kwa amani na watu wote, kadiri iwezekanavyo.” Na, kwa hiyo, tunataka kufanya hivyo.

<sup>15</sup> Na, sasa, kama hapakuwapo na mahali pengine mjini, au hamna mahali popote pa watoto kuchezea mpira, tungeona ikiwa hatungeweza kupazungushia ua mrefu, kote, ili mpira usipite na kuwasumbua na kuwakera majirani zetu. Lakini, papa hapa Ingramville, pale pale, wana kitovu cha uwanja wa mpira wa umma, kwa watoto wote, na viwanja vyao vya kuchezea. Juu tu ya Nane, pale makaburini, wana viwanja vya

michezo vya jiji zima pale, vya kuchezea mpira na chochote cha zaidi unachotaka kucheza.

<sup>16</sup> Sikufanya uamuzi. Nililitaja kwenye halmashauri ya kanisa, asubuhi ya leo, na kuwauliza linalotupasa kufanya, ili tudumishe amani na majirani zetu, na kuwa na marafiki zetu na kila kitu, nao watu wetu wangeelewa. Nao wameamua kuwa labda lingekuwa ni jambo jema kwetu kutowaruhusu wavulana kucheza mpira tena huku. Kwa sababu, ingekuwa . . .

<sup>17</sup> Si kama tunajali wakifanya hivyo; kanisa halijali, jamani, maskini dirisha dogo, taa mara moja moja. Lakini inatupasa kuwajali majirani zetu, pia, mwajua. Tunapaswa kuwajali. Nasi tunataka kuishi kama mabwana na mabibi Wakristo. Nasi tunaninii tu . . . Wataninii . . .

<sup>18</sup> Niliwaambia, njia tu wanayoweza kufanya, tungeweka tu ubao mdogo, kwamba wavulana hawapaswi kucheza mpira hapo. Nao . . . sisi . . .

<sup>19</sup> Sasa, ikiwa yeyote wenu majirani yuko hapa ndani, ambaye watoto wako wanacheza hapa kwenye ploti, nina hakika unaelewa, unaona, kwamba hatutaki simu zetu na kadhalika, na polisi huku, ama chochote kile, kuhusu kuvunja dirisha, taa na kadhalika.

<sup>20</sup> Nanyi wavulana wadogo, kama wavulana wenu wadogo wako hapa nje, na wasichana wadogo, wakicheza mpira, nao wanaona ubao huko nje, msininii . . . “Mpira usichezwe.” Vema, sasa, hatumaanishi kuwa wakali kwa watoto; lakini tunataka kuwaheshimu majirani zetu. Kila mtu ataelewa hilo, nina hakika.

<sup>21</sup> Nami nisingefanya uamuzi huo peke yangu. Niliomba halmashauri ije asubuhi ya leo, nikawauliza. Basi huo ulikuwa uamuzi wao, pia, wakifikiri kwamba tunapaswa kuishi kwa amani na ma—marafiki zetu.

<sup>22</sup> Na sasa wana nafasi ya mpira papa hapa, yapata tu mijengo miwili kutoka tulipo sasa, hiyo ni kitovu cha uwanja mkubwa mno, na kwa hivyo mnaweza kucheza mpira wote mpendao.

<sup>23</sup> Sasa, watu wanaotembea huku na huku kupitia huko, hiyo haimaanishi kwamba, kwamba wasipitie au chochote kile; itakuwa sawa kabisa.

<sup>24</sup> Na siku moja, natumaini, Bwana akipenda, na Yesu akikawia, kufanya se—sehemu rasmi ya kuegesha magari kwa ajili ya kanisa pale, ikiwa hatutajenga kanisa kubwa zaidi, na kuliweka. Na ikiwa siku moja . . . Mbona, kurudi, kwa hivyo litakuwa kubwa, tutakuwa na kazi hapa, mbona, mimi pamoja na Ndugu Neville sote tunaweza kuhusika nalo, na kadhalika. Tungejenga a . . . Tutumie tu sehemu hiyo kwa kanisa kubwa, na kujenga kanisa kubwa mno hapa, na kulitengeneza namna hiyo. Kwa hiyo, tu—tulinunua hiyo wakati tungeweza kununua.

<sup>25</sup> [Ndugu Roy Slaughter anazungumza na Ndugu Branham, akitoa lori lake kubeba mawe—Mh.] Asante, Ndugu Roy, hilo ni zuri sana, kama hilo, kama wanaweza kufanya uamuzi juu ya kulifanya. Endapo wataifanya kuwa sehemu ya kuegeshea magari, hilo lingekuwa ndilo jambo la kufanya. Hilo ni zuri sana. [Ndugu Slaughter anazungumza tena.] Naam. Naam. Naam.

<sup>26</sup> Watatuzuia kuyaegesha... Tunapo, tayari, upande mmoja wa barabara huko, kwa hiyo ita—itabidi tufanye maandalizi fu—fulani. Na kwa kweli, mahali hapa, sehemu hii ya maegesho hapa, hiyo ni ya jiji. Hiyo ni kweli. Ninii yetu... Ndio kwanza tupate kijishemu kidogo pale, si mbali *hivyo*, hata tuifikie barabara pale pale. Barabara kweli inapitia kwenye nyumba ya Brakeman pale, na inashuka moja kwa moja na kushika mle ndani. Hiyo ndiyo barabara ya kando. Maana, hili lilikuwa ni dimbwi, miaka mingi iliyopita, walipolijaza. Ndipo wakati uwanja wetu ulipopimwa, tuko moja kwa moja kando ya njia ya miguu, papa hapa, mnaona. Kwa hiyo, hatuna upande wa mbele. Hiyo ni hisani tu ya mji kule sasa. Na kwa hiyo hii itakuwa yetu, nyuma *hivi*.

<sup>27</sup> Kwa hiyo, basi, niko miongoni, kati, na kadhalika. Nami, loo, mimi ni u—u—upepo wa kimagharibi tu, naamini ndivyo wanavyouita, ama kitu fulani. Si—siwezi kutulia kwa chochote. Na, lakini, huenda ikawa siku moja Bwana atanena nami nije hapa na kujenga tu humu ndani, maskani kubwa mno, na kuwaruhusu watu kutoka sehemu mbalimbali waingie. Ikiwa ningejenga, tutalihitaji hilo. Kwa hiyo, mnaona, hatutaki kuliuza wala kuliharibu. Tukilihitaji, tutalijaza, na kulisawazisha hapa nje, na kuliweka kanisa juu, na vipandio vya kuingilia, na kila kitu. Basi hilo litashughulikia hiyo hali yote, mnaona. Na—nami nina hakika Bwana atatoa kila senti yake, wakati tu tutakapokuwa tayari kulijenga. Takriban eneo la dola mia moja hamsini, mia mbili elfu, na tupate vyumba vyetu wenyewe vya utangazaji na kila kitu papa hapa, na ibada ziendelee, wakati wote. Kwa hivyo, hatujui atakalofanya Bwana wetu. Tunayaombea tu mambo haya, na uinjilisti na kadhalika.

<sup>28</sup> Na wakati mwingine namwambia Bwana, “Vema, unaye Oral Roberts na Ndugu Allen. Na unao Billy Graham na hao wote huko nje. Nina faida gani kwa vyovyote vile?” Lakini ninii tu... .

<sup>29</sup> Sina budi kufanya tu kile anachoniambia nifanye, mnaona. Kwa hivyo, kidogo ninakaa kimya tu juu ya hilo. Sasa, kila mtu ataelewa hilo, nina hakika. Na Bwana awabariki.

<sup>30</sup> Sasa, hebu tuone. Imechelewa kidogo tu, kwa hivyo tutaweka shule ya Jumapili, labda, na mahubiri, pamoja, Ndugu Neville? [Ndugu Neville anasema, “Naam.”—Mh.]

<sup>31</sup> Nasi tuna furaha kusikia kuhusu mtoto wake, pia, sivyo? Jamani, mzima kabisa! Na kusema ni nabii mke. [Ndugu Neville anasema, “Ikiwa ni chochote.”—Mh.] Sawa. Vema, tuna—tuna

furaha kwa ajili ya hawa manabii wadogo wa kike, mnaona, na kila kitu. Ninamshukuru tu Bwana kwa ajili yao.

<sup>32</sup> Unajua, wanawake wanaongezeka hapa katika nchi, hata hivyo, mwajua. Hayo ndiyo tunayowazia, mnaona. Nadhani ni—ni kama watatu hadi watano. Watatu . . . Kati ya watoto watano wanaozaliwa, watatu kati yao ni wasichana. Nao wanawake wanazidi kuwa wakubwa; wanaume wanazidi kuwa wadogo.

<sup>33</sup> Wanawake wanachukua mamlaka. Bila shaka, huo ndio mwelekeo na unabii wa siku hizi, ya kwamba taifa hili ni taifa la mwanamke. Litaongozwa na mwanamke. Basi kumbukeni, thela- . . . mwaka wa 1933, niliona hilo likija katika ono, mwanamke mkuu mwenye nguvu atalitawala taifa zima, siku moja, hiyo ni kweli kabisa, kabla ya wakati wa mwisho, kabla ya maangamizi kamili.

<sup>34</sup> Magari, katika siku hiyo, yatakuwa na umbo la yai, yakionekana ni kama yanarudi nyuma, katika umbo hili hapo. Nayo yataendeshwa na nguvu za aina fulani, hata haitayabidi kutumia usukani, wakati mwingine. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] Kulitayarisha tu, na kuendelea namna hiyo. Mnaona, kabla ya maangamizi! Sasa, mnakumbuka, hiyo ni, sasa, hiyo iko kwenye kumbukumbu. Mnaona?

Nao wanawake watachukua mamlaka. Wanawake watachukua mamlaka.

<sup>35</sup> Na—na fundisho la kanisa Katoliki, ambalo daima nimesema lingetawala Marekani, liko karibu sana sasa hivi. Mnaona? Kumsujudia mwanamke, Mariamu, ambaye ni mungu mke, na ambalo ni kinyume na Biblia. Na kufanya maombezi kwa wafu, jambo ambalo ni kinyume na Biblia. Na mambo haya yote hapa, nayo yanasonga mbele moja kwa moja.

<sup>36</sup> Na wakati mwingine nafikiri, katika kujua mambo haya, kwamba imenipasa kuwa na mahali ambapo ningeweza kutulia na kuanza kufundisha, mnajua, na ku—kuendelea tu, hivyo. Na sasa, makanisani sasa, siendi ila saa chache tu na kuwaombea wagonjwa, kisha naondoka; na kuvuta tu, kuwaombea tu wagonjwa. Na kuna mengine mbali na kuwaombea wagonjwa, katika Biblia, mnajua. Naam. Mambo mengi ya—ya kufanya.

<sup>37</sup> Ninataka kutoa taarifa ya mkutano wa Canada, mojawapo ya mikutano bora sana ambayo tumewahi kuwa nayo katika bara la Amerika Kaskazini. Sijawahi, maishani mwangu, (Bw. Mercier ataiandika, na wengineo), sijaona jambo lolote likitukia kama yaliyotukia kwenye mkutano wa Canada. Na, bila shaka, Wapentekoste wamenikataa kabisa. Kila kitu kule kilikuwa ni Baptisti na Anglikana, na kadhalika. Kila mahali, Wapentekoste wamenikataa, kwa maana sitakubaliana na “ushahidi” wa Roho Mtakatifu, kama vile damu kutoka mikononi mwako, na mafuta yakitoka mikononi mwako, na mambo kama hayo, na kuona pinde za mvua, na mambo haya yote. Hisia hazina uhusiano

na wokovu, hata kidogo. Tunakuja kwa uchaji kwa imani. Tunamwamini Mungu, na—na ndivyo hivyo. Mnaona? Ndipo, basi, waliandika barua, awali, wakazituma Canada, ndipo Wapentekoste wakajitenga tu namna hiyo, lakini wasingekuwa na ushirikiano wala kuhusika katika mkutano huo, kwa maana nisingeukubali huo. Na kwa hivyo ningali. . .

<sup>38</sup> Haidhuru ni nani anayeukubali, ama chochote kile, mimi ninakaa na Biblia ya kale iliyobarikiwa. Amina. Hii ni Neno la Mungu. Na ikibidi tusimame peke yetu, tutasimama peke yetu, tujenge kanisa. Hiyo ni kweli.

<sup>39</sup> Sasa, kabla hatujalikaribia Neno La—Lake, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi wa maombi.

<sup>40</sup> Baba mbarikiwa, kweli tunakushukuru kwa ajili ya wakati huu wa ushirika pamoja kwenye Neno, na maagizo haya matakatifu ya Mungu. Basi jalia, tunapoyashiriki, kwa kuyasoma na kuyasikia, jalia Roho Mtakatifu ayavuvie mioyoni mwetu, hata, tukiondoka leo hii, tutasema kama wale waliotoka Emau, “Ni vema sisi kuwa hapa. Mioyo yetu iliwaka ndani yetu, kwa sababu alinena nasi njiani.” Tunaomba katika Jina Lake. Amina.

<sup>41</sup> Sasa, nimechagua, leo, yakiwa ni mapenzi ya Mungu, somo langu linapatikana katika—katika. . . katika Kitabu cha Zaburi, 63.

*Ee Mungu, wewe ndiwe Mungu wangu; nitakutafuta mapema: nafsi yangu inakuonea kiu, mwili wangu wakuonea shauku katika nchi kavu na yenye kiu, ambayo haina maji;*

<sup>42</sup> Msikilizeni tu mtunga-zaburi!

*Nizione nguvu zako na utukufu wako, ndivyo nilivyokutazama katika patakatifu pako.*

*Kwa kuwa fadhili zako ni bora kuliko uhai, midomo yangu itakusifu.*

*Ndivyo nitakubariki maadamu ni hai: kwa jina lako nitainua mkono wangu.*

*Nafsi yangu itakinai kama kushiba mafuta; na vinono, kinywa changu kitakusifu kwa midomo ya furaha:*

<sup>43</sup> Sasa Bwana wetu na aongeze baraka Zake kwenye Neno hili. Somo langu asubuhi ya leo linapatikana katika *U-h-a-i*, herufi nne ndogo.

<sup>44</sup> Na kama vile mtunga-zaburi hapa, alivyokuwa akisema, Daudi, daima Mungu hushughulika na mwanadamu sawasawa tu vile akili zao zinavyotenda kazi. Sasa, Mungu alishughulika na Daudi, kama malisho mabichi na maji matulivu, na kadhalika. Naye Daudi huko nje, baada ya kuona maisha mengi sana, jinsi Mungu alivyoishi katika mti, na jinsi alivyoishi katika

maua, na jinsi alivyoishi katika—katika mlio wa mawimbi ya kijito.

<sup>45</sup> Iwapo mtu yeyote aliwahi kuteremka kando ya kijito yalipo hayo maporomoko madogo, na kusikia sauti hiyo ya kimawimbi sikuzote. Loo, ninaweza kujilaza pale na kulala, kwa urahisi sana. Sijawahi kumeza kidonge cha kulala usingizi maishani mwangu. Nimejaribiwa kufanya hivyo, mara nyingi, katika mikutano yangu, wakati nimesongwa kabisa, lakini Mungu amenisaidia umbali huu. Lakini, nawaambia, ninaamini hiyo ingekuwa bora kuliko kila kidonge cha kulala usingizi ambacho wangekuwa nacho katika duka la dawa. Kulala tu kando ya kijito kinachotoa sauti ya kimawimbi, kijito kidogo, na kuomba kidogo, na, “Sasa najilaza chini,” na kulala tu hapo. Loo, kuna kitu kuhusu hilo ambacho hupumzisha. Jinsi ninavyokipenda!

<sup>46</sup> Naye Daudi hapa alisema, “Mimi ninaninii tu. . . Nafsi yangu inakuonea kiu tu!” Hebu sikilizeni.

*He Mungu, wewe ndiwe Mungu wangu; nitakutafuta mapema: nafsi yangu inakuonea kiu, mwili wangu wakuonea shauku katika nchi kavu na yenye kiu, ambayo haina maji;*

<sup>47</sup> Kisha anaendelea kusema:

*Kwa maana fadhili zako ni bora kuliko uhai, . . .*

<sup>48</sup> Sasa, inaonekana, hakuna kitu, bora kuliko uhai. Je, ni nini tunaweza kukadiriya asubuhi ya leo kingekuwa bora kuliko uhai? Lakini, Daudi anasema, “Fadhili zako ni bora, kwangu, kuliko uhai.” Sasa, tunashangaa, basi, neno uhai halina budi kuwa na ma—ma—maana ambatani kwake, halina budi kumaanisha zaidi ya—ya—ya jambo moja. Uhai, lenyewe, linamaanisha “maisha.” Kwa hivyo, basi, ikiwa “Fadhili zako ni bora kuliko uhai,” basi nini kinaweza kuwa bora zaidi? Kwa sababu, Mungu pekee ndiye aliye na Uzima wa Milele. Mungu pekee ndiye aliye na Uzima wa Milele. Tukiweza kuliweka hilo sawa sasa, itakuwa ni rahisi kwetu kuona ile picha kuu ambayo Mungu anaweka mbele zetu, jinsi ambavyo, siku moja, kwamba kila kitu ambacho si cha Mungu kitatoweka na kuangamia, na kuondoka.

<sup>49</sup> Sasa, kila kilichokuwa na mwanzo kina mwisho. Hakuna kilichoanza kisicho na mwisho. Lakini kitu ambacho hakikuwa na mwanzo hakina mwisho. Na—naye Mungu pekee Ndiye aliyekuwa “kamwe hana mwanzo.” “Hakuwa na mwanzo wa siku, wala mwisho wa miaka.” Na, kwa hiyo, inatubidi kuwa sehemu ya Mungu, kwa kuzaliwa, kuishi, kuwa na Uzima Milele.

<sup>50</sup> Kisha, dhambi na mateso, na kila kitu, lazima zifikie mahali ambapo hazipo tena, kwa sababu zilikuwa na mwanzo. Kulikuwa na wakati ambapo hapakuwa na magonjwa, hakuna dhambi, hakuna huzuni, hakuna mauti, ndipo basi yakaja kwa upotovu. Kwa hivyo, upotovu wote hauna budi kwisha kabisa. Na yote yaliyokuwako, yaliyokuwa na mwanzo, hayana

budi kwisha, kusudi yaliyo ya Milele yaweze kuwepo. Mnaona ninachomaanisha?

<sup>51</sup> Hiyo ndiyo sababu haiwezekani kabisa kwa mtu yeyote kuokolewa nje ya Kuzaliwa upya. Kwa sababu, wanadamu wanazaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, ndipo wanakuwa sehemu ya Mungu. Uwepo wao ni wa Milele kama vile Mungu alivyo wa Milele. “Kamwe hawawezi kuangamia,” Yesu alisema. “Hakuna awezaye kuwapokonya kutoka mkononi Mwangu. Wao ni wa Baba, wa Kiungu.” Wala hakuna mtu awezaye kuwachukua wala kuwatenganisha, kwa kuwa wao ni sehemu ya Mungu.

<sup>52</sup> Sasa hakuna wasomi kati yetu. Mimi—mimi ni mtu mwenye elimu duni sana. Lakini, wakati mwingine ninapoyafikia maneno kama hayo, ninayachunguza kweli kweli, nipate kujua, nachukua tu hilo neno moja. Ninao marafiki na walimu wa Biblia ambao wanaweza kuchukua Kiyunani, ama Kiebrania, na kukifuatilia popote katika Maandiko. Lakini mimi sina budi kulichukua neno kwa neno, na kulichunguza kabisa.

<sup>53</sup> Nami naona, ya kwamba, wakati Yeye aliposema, “Ninawapa Uzima wa Milele.” Linatokana na neno, neno la Kiyunani, Zoe, Z-o-e. Nalo Zoe ni Mungu, “Uzima” wa Mungu Mwenyewe. Na kisha, kwa hakika kadiri tulivyo washiriki wa Zoe, tunaishi Milele kama vile Mungu aishivyo Milele. Kwa hiyo, kwa kushiriki sehemu ya Mungu, tunafanyika waliobarikiwa na kuokolewa Milele, milele na milele, bila mwisho, bila mwanzo. Tunakuwa sehemu ya Mungu. Kama ukiangalia, ya kwamba mwanzo huu mkuu, hebu chukua . . .

<sup>54</sup> Kuna mtu fulani ameuliza swali, “Ni nani huyu Yehova mkuu? Alianzia wapi?” Hakuwa na mwanzo. Daima alikuwa ni Mungu. Naye ni . . .

<sup>55</sup> Sasa, neno *daima* linamaanisha tu “kipindi cha wakati.” Lakini, Umilele maana yake ni “daima.” Lakini, *daima*, neno *daima* katika Kiebrania, maana yake ni “kipindi, muda uliopangwa,” kwa kuwa liko katika wingi, “daima na daima.” Mnaona? Hiyo inamaanisha daima mbili. Unaona?

<sup>56</sup> Lakini, katika Umilele, ni umoja, kamili. Umilele ni du—duara isiyo na mwisho. Haikuwa na mwanzo wala haitakuwa na mwisho.

<sup>57</sup> Na jinsi ambavyo, katika ulimwengu, tunajua kwamba kuna roho halisi, ya kweli ya upendo. Kuna roho halisi, ya kweli ya uaminifu. Kuna roho halisi, aminifu ya ukweli. Ni wangapi wanaojua hilo? Tunajua hilo. Tunaliona. Vema, huyo ni Mungu, che—chemchemi yenyewe.

<sup>58</sup> Hebu tufunge macho yetu, kwa mawazo yetu, kwa dakika chache, na turudi nyuma kabisa katika . . . kabla hakuwajuwako na chochote.



59 Ile chemchemi kuu ya Umilele wote ilikuwa ni hiyo Roho ya upendo, furaha, Roho hiyo ya uaminifu, hiyo Roho ya ukweli, katika ukamilifu huu. Ndipo basi, kutoka kwa kuwepo kwa Baba, ikatoka Logos, ambayo ilikuwa ni Mwana, ambaye alikuwa Thiofania, ambayo ilikuwa ni Mwili wa Yehova Mungu mkuu, akatokea katika Mwili wa kimbinguni. Hiyo ndiyo Logos. Neno lilinena kutoka katika hizo chemchemi kuu za Uzima, kisha likatoka. Na kulikuwa na—na Thiofania, ambayo ilikuwa ni Mungu aliyefanyika Neno.

60 Ndipo hiyo Thiofania ikafanyika mwili, katika utu wa Kristo Yesu. Ndipo basi utimilifu wote wa utatu ukakaa ndani Yake, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, wote katika huyo.

61 Na hivyo ndivyo tunavyoenenda hasa, moja kwa moja hadi kwenye mwanzo asilia, wa Mungu. Hapo tunazaliwa mara ya pili, si kwa mwili; tunazaliwa mara ya pili, si kwa damu; bali tunazaliwa mara ya pili kwa Roho. Na katika huyo Roho wa Milele wa upendo na uaminifu, anashuka kujitengenezea mahali Pake ndani yetu.

62 Na kisha tunapokufa, kutoka kwa maisha haya, tunaingia katika huo mwili. “Ambapo, kama nyumba ya maskani hii iliyo ya dunia ikiharibiwa, tunayo thiofania ya kuendea, mwili wa mbinguni.”

63 Kisha, katika Kuja kwa Bwana Yesu, mwili huu utanyakuliwa kutoka duniani tena, na kufanywa katika hali ya utukufu, upate kuishi katika Uwepo Wake milele.

64 Ndipo, upotovu wote, mambo yote yaliyokuwa katika ule upotovu, yote yanatoweka. Mwili unaenda kwenye adhabu yake. Kuzimu inafungua kinywa chake na kumeza maovu yote na upotovu. Naye Mungu na Kanisa Lake pendwa, Bibi-arusi Wake, wanachukua msimamo wao Milele isiyo na kikomo. Hilo ndilo tumaini kuu la Kanisa la Kikristo.

65 Naye Daudi alipiga kelele, “Ee fadhili Zako ni bora kwangu kuliko uhai.”

66 Sasa, uhai, kila mtu anataka kufikiria juu ya uhai. Nayo maisha, neno *maisha*, limekuwa na kipengele kilichopotoshwa, kwa sababu hata maisha yenyewe yana kipengele kipotovu. Na mara nyingi, watu wanataka kuyanena maisha kwamba ni kuwa na wakati mzuri sana, kunywa pombe, kujifurahisha, na kutoka nje. Wanasema, “Haya ndiyo maisha.” Jinsi walivyokosea. Hayo ni mauti. Mnaona? Sio maisha. Ni mauti.

67 Majuma machache yaliyopita, katika hoteli nzuri, maarufu huko—huko Canada ambapo walikuwa wameniweka. Nilipanda chumbani kwangu, baada ya ibada yangu. Na kulikuwako na wasichana, labda kwenye mwisho wa utineja wao, umri wa miaka kumi na minane, kumi na tisa, labda hadi ishirini na mitatu, kitu kama hicho. Watatu kati ya wanne wao wakikimbia huku na huku sakafuni, wakiwa tu na mavazi yao

ya ndani. Huku wameshika chupa mikononi mwao, wakikimbia kutoka chumba kimoja hadi kingine, wasichana wenye sura za kupendeza.

<sup>68</sup> Nilipokuwa nikishuka kwenye lifti, nilisimama na kuangalia. Loo, kulikuwako na kitu Fulani ndani yangu! Nikawazia, “Ee Mungu, je, mtoto wangu Rebekah ama Sarah kamwe watafikia hayo?”

<sup>69</sup> Nami nikawatazama. Waliyumbayumba sakafuni. Nikaingia tu, upande mmoja, nao wakapita na kuendelea, wakapitia kwingine, wakinywa pombe. Nikasimama, kupitia ukumbini, nikatazama chini tena, nikaona maskini wasichana warembo ambao pengine wangeweza kuwa wapenzi halisi wa wanaume fulani. Ndipo nikamsikia mmoja wao akisema, “Whoopii! Haya ndiyo maisha!”

Nikawazia, “Ni kosa la jinsi gani! Hayo ni mauti.”

<sup>70</sup> Kwa kuwa, Biblia ilisema, “Yeye anayeishi kwa anasa amekufa ingawa anaishi.” Kwa hiyo basi tunaona, kwamba maisha, kile tunachokiita maisha.

<sup>71</sup> Na tunaona mabango siku hizi, kama hili, “Palipo na Budweiser, pana maisha.” Ni upotovu ulioje huo! Palipo na Budweiser, ni mauti.

<sup>72</sup> Na tunaona vibango kama hiki, pia, “Maisha huanza jua linapotua.” Hapana. Mauti huanza jua lituapo. Watu wanakuwa wazururaji usiku. Wanazurura usiku. Na ukiangalia, wanachukua asili ya uovu. Uovu daima huzurura usiku.

<sup>73</sup> Nami nilisoma makala katika gazeti, wakati mmoja nilipokuwa kwenye ndege. Ilikuwa ni kuhusu Hollywood. Nayoyakasema, kwamba, “Maisha huanza baada ya usiku wa manane. Unapaswa kuja kwenye mitaa fulani na vitu fulani.” Nayoyalikuwa na picha ya vichekesho, na kadhalika, vinavyoendelea.

Nami nikasema, “Ni upotovu jinsi gani huo!”

<sup>74</sup> Mnaona, ikiwa Shetani ana ufalme, hana budi kuwa na uchumi wa uongo. Hana budi kuwa na kitu anachoweza kuwasilisha kwao, kuwafanya wafikiri wanaishi. Lakini kiko upande huo mwingine kabisa. Ni mauti, katika mfano wa maisha. Mnaona? Ni upotovu kutoka kwa maisha halisi.

<sup>75</sup> Kwa sababu, hebu tulitatie jambo hili niani mwetu sasa, mara moja tu. Kuna njia moja tu ya kuwa na maisha. Hiyo ni kweli. “Na kumjua Yeye ni Uzima.” Hiyo ndiyo njia pekee tunayoweza kuwa na Uzima, wala hakuna njia nyingine, kwa maana Mungu ameahidi tu Uzima kupitia Yesu Kristo. Naye Yehova mkuu, asiye na mwanzo wala asiye na mwisho, asiye—asiye na mwanzo wa siku wala mwisho wa miaka, ametupa Uzima kwa njia ya Yesu Kristo, na Yeye pekee.

<sup>76</sup> Sio tu kumtambua kama mtu mwema; si kumwabudu tu kwamba Yeye pengine angekuwa, ki—ki—kijimungu, ambapo Yeye ndiye Mungu. Lakini, jambo la kufanya ni kumjua Yeye. Jambo ndilo hilo. Si kumwabudu Yeye, bali, “Kumjua Yeye ni uzima.” Mashetani walimsujudia. Bila shaka. Kila goti litapigwa Kwake.

<sup>77</sup> Lakini, “kumjua Yeye,” katika kusamehewa dhambi zako, na kufanywa upya kwa maisha yako, kwa Roho Wake, chemchemi hiyo kuu ya rasilimali yote ya wema ikikaa ndani yako. Mungu akikufanya uzae matunda ya upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, upole, utu wema, uvumilivu, imani, na sifa hizo zote kuu zinazotoka kwa Mungu pekee. Hiyo ndiyo njia pekee ya kuwa na Uzima.

Kwa hiyo, neno *maisha* limetafsiriwa vibaya kwetu.

<sup>78</sup> Sasa, sisi, kile tunachoita maisha, mtu atapata gari jipya, au watashuka barabarani, nao watafurumisha tu, labda, wakiwa wamelewa, na mkono wao umemkumbatia msichana, na kisha jamaa mdogo aseme, “Haya ndiyo maisha!” Naye huyo msichana, pamoja na mvulana rafiki yake aliyemchagua, naye amekunywa chupa moja au mbili, naye atasema, “Haya ndiyo maisha!”

<sup>79</sup> Au, labda mtu ambaye sikuzote ametaka pesa nyingi, na, kwa ghafla, anafanywa mrithi wa kiasi kikubwa cha fedha. Atajenga nyumba nzuri sana. Atapata gari bora zaidi. Atapiga makelele, “Haya ndiyo maisha!”

<sup>80</sup> Maskini mwanamke mfua nguo pamoja na watoto wake. Atapata safari ya kwenda Hollywood, naye atakuwa “malkia kwa siku moja,” kwenye kipindi fulani, au baadhi ya mambo hayo, au kushinda sehemu ya bidhaa. Itamfurahisha sana, hadi kufikia mahali atakaposema, “Haya ndiyo maisha!”

<sup>81</sup> Lakini jinsi ilivyopotoshwa! Hayo ni mauti. Na wale walio nayo wataangamia. Nasi tunaona, siku hizi . . .

<sup>82</sup> Sasa kidogo tu ninaweza kuwa wa mtindo wa kale juu ya mambo haya, na kwa namna fulani nikate kona na kuponda kwa nguvu, lakini kweli ni . . . Makusudio yake, ni kuonyesha hoja.

<sup>83</sup> Sasa, wengi, siku hizi, wanatazama kipindi. Wanasikiliza rekodi. Wanaingia kwenye mikahawa midogo, na ni vigumu kwako kula kwa—kwa ajili ya rekodi mashuhuri wanazocheza, za hii roki na—na bugi-bugi, na rekodi hizo zote za kimapenzi, dansi chafu, zilizobuniwa na kuvuviwa na ibilisi. Na, loo, nashangaa matokeo ya mwisho yatakuwa nini watakapopata kujua kwamba hayana uhusiano na Yule wa Milele!

<sup>84</sup> Ninawazia, siku hiyo hapo jua litakapokataa kuangaza, na wakati wote usimame kimya na kuyeyuka katika Umilele, nitawazia Elvis Presley atatetemeka sana, kwenye asubuhi hiyo. Hapana shaka. Naam. Santuri zake zitadhihirika, atakaposikia

vilio vya mamilioni ya watu aliowapeleka kuzimu. Vile vipande thelathini vya fedha vya usaliti wa Yuda vikialika kwenye sahani, itakuwa starehe, ikilinganishwa na wakati wa hukumu ya Elvis Presley, asubuhi hiyo. Kwa maana, Yuda alifanya hivyo kwa sababu ilikuwa ni kutimiza Maandiko, kumkomboa mwanadamu. Lakini Elvis Presley alipotosha kilicho sahihi, wakati yeye akiwa ni Mkristo, naye akauza haki zake za mzaliwa wa kwanza kwa watu milioni moja kuzimuni.

<sup>85</sup> Ninawazia, Arthur Godfrey, pamoja na maskini akina Godfrey wake wadogo wote, watakuwa huko asubuhi hiyo, pia, na nywele zake nyeupe, za kahawia, na nyekundu. Na itachukua zaidi ya “salamu Maria” kuweza kuisafisha nafsi yake chafu na dhamiri yake, Mbele za Mungu. Anapojisikia, kwamba, ile mizaha michafu na dhihaka, na kadhalika ambapo amewaongoza mamilioni kuzimu, kwayo.

<sup>86</sup> Nao wanayaita hayo, “Maisha.” Mbona, ni mauti, wala hawajui.

<sup>87</sup> Sasa angalieni, katika hili, jambo hili mnaloliita “maisha,” linakuwa la huzuni sana mpaka, mara nyingi, watu wanajiuu. Kwa hiyo, hayo hayawezi kuwa ndiyo Maisha ambayo Mungu anazungumzia, kwa maana huwezi kuuchukua Uhai wa Mungu, wala pia huwezi kuutoa Uhai wa Mungu. Hilo liko kwa neema kuu mikononi mwa Mungu pekee. Lakini maskini kitu hiki kidogo kinachopatikana na mauti unachoishia, kiitwacho uhai, unaweza kukitoa hicho unapotaka. Lakini, unaonyesha kwamba hayo si Maisha! Yanakuwa yenye mashaka jinsi gani!

<sup>88</sup> Haya tunayoita maisha sasa, ni kivuli tu au hasi. Sisi sote tunapenda kushangilia, lakini tunaweza kushangilia juu ya jambo linalofaa. Hiyo inaonyesha kwamba tumeunganishwa na kitu halisi, tunapofurahia jambo lifaalo. Lakini tunaposhangilia jambo baya, inaonyesha kwamba tumeunganishwa na jambo baya. Kwa hivyo, maisha yetu yanaweza kuonyesha sasa hivi sisi ni nini, kule hisia zetu zinaelekea. Mnaliona? Sisi ni . . .

<sup>89</sup> Ikiwa tunaufurahia ulimwengu na mambo maovu, akili zetu na roho zetu zinaongozwa kutoka chini. Bugi-bugi, madansi, huzuni, kunywa pombe, mambo haya mengine yote tunayokimbilia, yanatoka chini.

<sup>90</sup> Lakini kama tukifurahi katika Roho, ya kwamba tuna Uzima wa Milele, na tumwinulie Mungu hisia zetu na kumsifu, basi tunayo furaha. Basi tuna furaha. Yesu alisema, “Mimi . . . ili furaha zenu zitimilike.” Lakini, sio kujazwa na maisha yaliyopotoshwa, bali kujazwa Uzima wa Milele, huko Juu. Kwa hiyo, mnaweza kuona, inategemea kile unachoangalia.

<sup>91</sup> Sasa kwa mfano tu, kwa sehemu yake ya saikolojia, kiakili; sasa hebu tuangalie, kwa muda kidogo tu, mtazamo huu wa kiakili. Hii *hapa* picha ya Kristo, na hii *hapa* feni ya umeme. Inategemea ni ipi ninayoangalia, mnaona, kama hisia zangu

zinasogezwa *huku* au hisia zangu zinasogezwa *huko*. Nikiangalia *ile*, na kutamani ile na kutaka ile, hisia zangu zimeelekezwa kwenye feni. Lakini nikiangalia *huku*, hisia zangu na shauku zangu zinaelekezwa hivyo.

<sup>92</sup> Hiyo ndiyo sababu Yesu alisema, “Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Unaona? Ni pale ambapo hisia zako zimewekwa, mahali mawazo yako yalipo.

<sup>93</sup> Ndipo tunaweza kufurahi kwa sababu sisi tu watoto wa ile ahadi, juu ya Kanisa kuu la Milele la Mungu, ambalo lina ahadi ya Kristo Mwenyewe, “Haliwezi kushindwa.” Hiyo ni kweli.

<sup>94</sup> Ulimwengu unafikiri sisi ni wazimu. “Loo, *haya* ndiyo maisha! Whoopii!”

<sup>95</sup> Leo hii ninapaswa kumwona msichana ambaye alienda kwa . . . Naye daktari wa akili . . . Ana umri wa miaka thelathini na mitano; hajawahi kuvuta sigara, hajawahi kunywa pombe, maishani mwake mwote. Msichana mzuri sana. Watu wake ni Wakristo. Baba yake ni daktari. Naye alikuwa . . . aliyatoa maisha yake kwa Kristo, mapema. Basi alifanya nini? Anatoka, na hatimaye anafikia mahali ambapo anaenda kwenye chuo alichokuwa akifundisha. Naye daktari wa magonjwa ya akili huko, akaketi chini kuzungumza naye, naye akasema, “Unamaanisha kuwa hujawahi kubusiwa na mvulana?”

Akasema, “Si hata wakati mmoja, maishani mwangu mwote.”

<sup>96</sup> “Unamaanisha hujawahi kunywa pombe kidogo na kuhudhuria karamu?”

“La, hasha.”

Kasema, “Ewe msichana, hujui unachokosa.”

<sup>97</sup> Sasa, yeye akiwa daktari wa magonjwa ya akili, aligeuza mawazo ya msichana huyo, mpaka sasa amekuwa mvovu sana na mbaya sana, mpaka hata hataki kusikia Jina la Yesu likinenwa mbele—mbele yake. Na hata baba na mama yake hawawezi kumwona, tena. Naye ameingia wazimu, na juma hili lilalo atakwenda hospitalini kwa tiba ya kushtuka kwa mishipa. Ni kwa sababu aliondoa mawazo yake kwa Kristo, akayaelekeza kule huyo daktari wa magonjwa ya akili alikuwa akielekeza mawazo yake.

<sup>98</sup> Na hilo ndilo lililotuleta hapa, asubuhi ya leo, ni kuiondoa nia yako na mawazo yako kutoka kwa mambo ya ulimwengu, mpaka mambo ya Mungu, ambayo ni ya Milele. Na hiyo ndiyo sababu ya kuhubiri, ni kuyageuza mawazo ukayaweka mahali pa juu na bora zaidi, na mahali alipo Kristo, mpaka uwe umeongoka. Ndipo nia yako inayafikia mambo yaliyo Juu.

<sup>99</sup> Sasa, lakini maisha katika mahali hapa pengine, yakimfikia huyo msichana, wanafikiri huenda akanywa sumu wakati

wowote. Hakika, maisha yanakuwa yenye mashaka sana, aina hiyo ya maisha, mpaka wanajiua wenyewe, wanakunywa sumu na kila kitu.

<sup>100</sup> Sasa, lakini, Mungu, katika uchumi Wake mkuu kwa wanadamu, amemfanya mwanadamu kwa njia ambayo Yeye alitaka mwanadamu awe. Sasa, Yeye alimfanya mwanadamu kuona kiu.

<sup>101</sup> Je, mlimwona Daudi hapa? Kasema, “Nafsi yangu inakuonea kiu.” Loo, ninapenda hilo. “Kama katika nchi kavu, ambako hakuna maji.” Hebu wazia. Kasema, “Nafsi yangu ina kiu sana, Mungu! Ninakuonea kiu, jinsi tu ningekuwa katika nchi isiyo na maji.” Lazima atafute maji la sivyo aangamie. “Nafsi yangu inakuonea kiu.”

<sup>102</sup> Sasa, Mungu alimwumba binadamu akiwa na kiu. Hiyo ni sehemu ya mwanadamu, ni kiu yake. Lakini, Mungu aliumba kiu ndani ya mwanadamu apate kumwonea Mungu kiu. Naye ibilisi ameipotisha, na kuifanya kiu ya ufalme wake, kwa ajili ya ulimwengu. Je, mnalipata? Kiu ndani ya mwanadamu ni ya kiungu, kwani Mungu alimwumba mwanadamu apate kuona kiu, kiu ya Mungu.

<sup>103</sup> Basi baadhi yenu mnathubutuje, ambao mngekuwa duni sana hata mkalia . . . kujaribu kuzima kitu hicho kilichobarikiwa cha kiu, kwa kujaribu kuridhisha hicho kwa kunywa pombe, na kuvuta sigara, na televisheni, na kukimbia na kufanya yasiyofaa, na shamrashamra za huku na huku, ukijaribu kukidhi kitu hicho cha kiungu ambacho Mungu aliweka ndani yako kumwonea kiu. Unachafua chemchemi ambayo Mungu ameweka ndani yako, kumpokea Roho Wake, nawe unaizamisha kwa mambo ya ulimwengu. Wala hayaridhishi. Kamwe hayataridhisha.

<sup>104</sup> Na hiyo ndiyo sababu unalenga bastola kwenye bongo zako, kuzilipua, ni kwa sababu mambo yanaenda jinsi yanavyoenda. Nao ulimwengu umeingia katika kujiua kukuu, kwenye upotovu na ushoga, na uhalifu uko nchini jinsi ulivyo, ni kwa sababu mnapotosha kitu chenyewe ambacho Mungu aliwapa, na kujaribu kukiridhisha na uovu wa ulimwengu.

<sup>105</sup> Unamchukua huyo Roho Mtakatifu mbarikiwa, ambaye Mungu aliweka kiu nafsi mwako ya kumwita, nawe unairidhisha na klabu ya usiku mahali fulani, si ajabu unaumwa na kichwa kesho yake asubuhi. Kisha, utachukua sa—sanduku la bia na kwenda nyumbani kwako, unaketi na kuinywa, ukijaribu kuridhisha ile kiu ya kiungu ambayo Mungu aliweka nafsi mwako upate kumwonea kiu. Kisha unayachukua matapiko ya ibilisi na kujaribu kuridhisha ki—kiu ambayo Mungu aliweka ndani yako, kumwonea kiu, unawezaje kupokea chochote ila utengano wa Milele kutoka Mbele za Mwenyezi Mungu! Wakati, Yeye alikuumba umwonee Yeye kiu!

<sup>106</sup> Naye Daudi akajisalimisha, akasema, “Nafsi yangu inaona kiu, kana kwamba nilikuwa katika nchi kavu isiyo na maji. Ninakuonea Wewe kiu, Ee Mungu.” Haya basi. Daudi akasema, “Nilikuona katika patakatifu Pako, nayo nafsi yangu inazionea kiu Nguvu hizo.” Haya basi. Hiyo ndiyo tofauti. Hilo ndilo linalofanya mambo kuwa tofauti, ni kiu ambayo Mungu alikupa, kama ukiiridhisha kwa Maji.

<sup>107</sup> “Njoni Kwangu, ninyi nyote mlio na kiu. Njoni mzinywee chemchemi za Uzima, bure, bila fedha, bila gharama. Kuna chemchemi iliyofunguliwa katika Nyumba ya Mungu, katika mji wa Daudi.”

<sup>108</sup> Hiyo hapo Chemchemi unayoionea kiu. Hakika, ndiyo hiyo. Usijaribu kuipotosha, kwa kujaribu kusema, “Nitairidhisha, kwa kunywa pombe. Nitairidhisha, kwa kuweka miadi na msichana *huyu*. Nitamkimbia kidogo mume wangu. Nitamkimbia kidogo mke wangu.” Unajilimbikizia tu hukumu!

Unasema, “Sijaridhika, Ndugu Branham.” Si ajabu!

<sup>109</sup> Ni Mungu akishughulika nawe. Mungu akijaribu kukuleta kwenye kitu fulani, nawe unachukua pendekezo la ibilisi na kuondoka nalo. Na hivyo ndivyo huzuni inavyokuja. Ndivyo kifo kinavyokuja. Na maisha hayo si Maisha; ni mauti. “Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni Uzima wa Milele kwa hao watakaoupokea.” Loo, usidanganyike.

<sup>110</sup> Kisha, ibilisi ana njia nyingine. Tuna muda mfupi tu, bado, kwa hili. Ibilisi anayo njia nyingine ya kupotosha, mbali na hiyo. Kusema, “Ninasema sinywi, Ndugu Branham, sivuti sigara. Sichezi kamari. Nisingemdanganya mume wangu au mke wangu. Ni—nitafanya. . . Ninaishi maisha mazuri.” Lakini ibilisi ameipotosha hiyo. Anakuacha ufikiri, kuridhisha dhamiri yako yenye hatia, ya kwamba uende ujiunge na kanisa nawe uko sawa. Hilo ni kosa. Huko ni kupotosha. Huwezi kupata utoshelevu kwa kujiunga na kanisa. Unakuwa tu wa kiakili; ni jambo la kiakili.

<sup>111</sup> Lakini kamwe hutaridhika mpaka utakapomjua Yeye, kwa msamaha wa dhambi zako, ambapo swali la dhambi linatatuliwa, nawe una ushirika huo wa kupendeza, wa amani, mtulivu, wa Milele pamoja Naye. Wakati amani ya Mungu ipitayo ufahamu wote imeitakasa nafsi yako na imekufanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Kujiunga na kanisa hakutafanya hivyo. Hapana, bwana. Huko ni kupotosha tu sababu halisi. Iwapo ibilisi hawezi kukuingiza kwenye mambo hayo, atakupeleka kwenye haya mengine. Lakini usikubali chochote pungufu ya tukio la mtindo wa kale la Kuzaliwa upya, kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu wa Milele. Hapo nafsi yako na Mungu mnapoungana mkawa kitu kimoja.

<sup>112</sup> Daudi, pia, katika Zaburi, akiwa mtu wa m—msituni na mwindaaji.

113 Huko Kusini wangali wanawatumia, makundi ya mbwa mwitu kuwawinda kulungu, mara nyingi. Na katika Afrika nimeliona. Basi kulungu wanapoanza kukimbia, mbwa-mwitu huwauma. Nao wana meno makali sana ya mbele. Basi wananyemelea kimya sana, kama dhambi. Wanamvizia maskini huyo kulungu. Wanaukabili upepo ili asiweze kusikia harufu yao. Nao wanatoka, kwa ghafla, na kumvamia maskini jamaa huyo, na kumrarua vipande-vipande.

114 Hivyo ndivyo dhambi ifanyavyo. Inakupeleka kwenye uwanja mwingine. Unapofikiria kwamba, wewe, “Vema, nitajaribu *hii* kidogo tu. Nitapita na *hii*. Mimi... Kamwe hawatawahi kujua lolote kulihusu, *hili, lile*.” Usijali, kuna Jicho lionalo yote linalokuangalia. Na dhambi iko mlangoni. Kuwa mwangalifu. Itakupata.

115 Halafu wakati mwingine maskini kulungu anapokamatwa, labda wakati mwingine huwakamata ghafla upande wa nyuma. Labda wasiwafikie juu vya kutosha kuwaangusha chini. Wanawakamata ghafla ubavuni na kung’wafua kipande kizima. Na labda, basi, atamkamata ghafla, ili avunje ukano wa mvungu wa goti lake la mguu wa nyuma *hapa*, ambalo litamvunja, ndipo asiweze kukimbia. Hajiwezi.

116 Lakini wakati mwingine atapanda juu sana, na kumkamata nyongani, na kung’wafua kipande kizima, namna *hiyo*, ambapo mbwa humfikia tu na kumkamata ghafla, na kumgonga kwa uzito wake, na kung’wafua kipande kizima. Labda atakosa mshipa wa shingo kooni mwake, na kumkamata ghafla kwenye kidari na kung’wafua kipande kizima. Naye maskini, jamaa huyo mdogo akiruka na kukimbia upesi awezavyo, na, muda si muda mwajua, amewachenga mbwa na amewapumbaza. Mbwa wanakimbilia kitu kingine, naye anatumia mbio. Anajua itachukua tu muda mfupi, mpaka mbwa hao, mara tu watakapomwua huyo mwingine, watamfuatilia mara moja. Ndipo anakimbia, upesi awezavyo.

117 Sasa, nikiwa mwindaji, ninawafahamu kulungu. Ninafahamu matendo yao. Na ukiona, mradi kulungu anaweza kupata maji, ndugu, anaweza kupata nguvu mpya katika sekunde moja. Lakini asipoweza kufikia maji, amekwisha. Lakini akiweza kuyafikia maji, ungeweza kumfuata siku nzima, naye atazidi tu kwenda mbele. Ataingia kwenye kijito; atakivuka *hivi*, na atarudi *hivi*. Atarudi *hivi*. Atashuka mtoni na kutembea. Anajaribu kuwapumbaza mbwa.

118 Sasa, Daudi alisema, “Kama ayala auoneavyo shauku mto wa maji, vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea kiu, Ee Mungu.” Amejeruhiwa. Mbwa wa kuwindia wa kuzimu wanafuata kila mmoja wenu. Anataka tu kukuondoa kwa Mchungaji, mara moja tu. Nao wanawanyakua na kuwakamata ghafla konzi moja *hapa*, na funda moja *hapa*, ili kuwakwamisha. Ndipo Daudi akasema,



“Kama ayala anavyokionea shauku kijito cha maji!” Loo, hana budi kupata kijito cha maji, la sivyo, aangamie.

<sup>119</sup> Mungu, jalia hiyo iwe nafsi yetu leo hii! Kujeruhiwa, “Nisipoweza kupata kijito cha maji, hao mbwa wa kuwinda watanipata upesi sana. Lakini laiti ningaliweza kupata kijito Chako cha maji, Ee Mungu!”

<sup>120</sup> Maskini huyo kulungu anajua ama...Ni mauti au kijito cha maji. Naye Daudi alisema, “Kama vile tu kulungu huyo anavyojua ni mauti, ama kijito cha maji, hivyo ndivyo nafsi yangu inavyokuonea Wewe kiu. Sina budi kukupata Wewe, la sivyo niangamie.”

<sup>121</sup> Loo, laiti tungeweza tu kuyafikia Maisha ya namna hiyo! “Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana watashibishwa.”

<sup>122</sup> Jalia hizo ziwe ndizo nia za kanisa hili asubuhi ya leo. Shauku zenu na zigeuzwe kutoka kwenye mambo ya ulimwengu, shughuli za ulimwengu. Iwe ni nyumba yako inayosafishwa, iwe ni shamba lako linapaliliwa, au chochote kile, na zielekezwe kwa Mungu. “Ee Bwana, fadhili Zako za upendo ni bora kwangu kuliko maisha yote. Nafsi yangu inakuonea kiu, kana kwamba nilikuwa katika nchi kavu. Na kama ayala kwa kijito cha maji, nafsi yangu haina budi kukupata Wewe, la sivyo itaangamia.”

<sup>123</sup> Wakati Maskani ya Branham itakapofika mahali hapo, maskini hizo itikadi zitaanguka kutoka milangoni, tofauti zote zitatatuliwa, nao Wakristo watakuwa Wakristo. Na ninii... Hili litakuwa eneo ambalo litazungumziwa, kote ulimwenguni, wakati kusanyiko lolote la watu litakapomwonea Mungu kiu kwa njia hiyo. “Fadhili zako za upendo, Ee Bwana, ni bora kwangu kuliko uhai.”

Na tuombe.

<sup>124</sup> Baba yetu mbarikiwa, na Mungu, tunapokuja Kwako sasa mwishoni mwa Ujumbe huu mfupi, tunaomba ya kwamba kuona njaa na kiu kutakuwako katika kanisa hili dogo, asubuhi ya leo, kuliko hapo awali. Jalia wanaume, wanawake, wavulana kwa wasichana, leo hii katika... chini ya paa hapa, na nje, au popote wawezapo kuwa, na waisikie Injili, na kujua ya kwamba kuna kitu ki—kinachowafanya kuonea kiu kitu fulani.

<sup>125</sup> Loo, ghasia kama hizo! Ulisema itakuwa kwenye wakati kama huu, “ghasia, mshangao wa wakati, dhiki kati ya mataifa.” Loo, laiti wangechukua shauku hiyo ya kupata nguvu zaidi, shauku ya mabomu zaidi, shauku ya vitu hivyo, na kuigeuza kuwa shauku ya haki ya Mungu, basi Jua la Haki lingekuja na uponyaji katika mbawa Zake.

<sup>126</sup> Na wakati Israeli walipoona utungu, ndipo watoto walipozaliwa. Nami naomba, Baba, ya kwamba utaweka hiyo kiu mioyoni mwetu leo, kwamba hakuna utoshelevu popote ulimwenguni, isipokuwa tu kwa sauti ya maporomoko ya maji

Yako. Ee Bwana, jalia kilindi kiite Kilindi. Tujalie, Baba. Tunaomba katika Jina la Kristo.

Basi huku tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu.

<sup>127</sup> Sijui, kanisani, asubuhi ya leo, kama mtu fulani angeinua mkono wao, aseme, “Ndugu, mchungaji, uniombee,” sasa wakati mimi na Ndugu Neville tunapoangalia. Mungu akubariki, ndugu. “Namtaka Kristo. Nataka kiu kama hiyo moyoni mwangu. Nimechefuka sana na nimechoka kwenda huku na nusunusu kwenda *huku na kule*. Hakika nataka kuona kiu ya kumtafuta Mungu. Niombeeni, ndugu, wachungaji. Sivyo. . .”

<sup>128</sup> Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, mama. Na Mungu akubariki, ndugu. Mtu mwingine inua mkono wako, useme, “Niombee.” Kama. . . Mungu akubariki, dada. Vema. Mtu mwingine sasa, kabla tu ya kufunga, inua mkono wako, useme, “Niombee.” Mungu akubariki, mama. Bila shaka. “Nataka, pia.” Mungu akubariki, dada, huko nyuma. Hebu. . .

“Kwa sauti ya maporomoko ya maji Yako.”

<sup>129</sup> “Ee Mungu, nifanye—nifanye—nifanye nijue kuwa mimi ni mtu dhaifu, kwamba, sijui ni wakati gani hasa nyuzi hizi ndogo dhaifu za maisha zitakapokatika, nami ninatoka kwenda katika Umilele. Lakini nijalie, Ee Mungu, hata nafsi yangu ikuonee kiu sana, hata sitataka tena kunywa pombe, kuvuta sigara tena, kusema uwongo tena, sitaki tena kuhusiana na dhambi. Shauku zangu ziwe juu ya mambo ya juu. Nijalie, Ee Mungu, ninapoinua mkono wangu.”

<sup>130</sup> Mungu akubariki, na wewe, na wewe, na wewe. Mungu awabariki. Baba anauona mkono wako; hakika, Mu—Mungu aliye kila mahali. Mungu awabariki. Ungama tu sasa hivi, huku umeketi hapo. Kiri tu, useme, “Bwana, weka kiu hiyo ndani yangu.”

<sup>131</sup> Watoto, je, mnajua hili, kwamba hamtamfikia Mungu kwa chochote pungufu ya hiyo? Je, hiyo ni kiu ile kubwa, kile—kile kitu fulani ambacho kina shauku ya Mungu?

<sup>132</sup> Kama tu maskini yule kulungu, ungeweza kumwazia? Amejeruhiwa. Yuafa. Ni ama kijito cha maji au mauti. Naye hana budi. . . Je, ungeweza kumwona akiinua maskini kichwa chake? Naye ananusanusa. Ananusa hewa. Damu inatiririka. Hana budi kukifikia hicho kijito cha maji. Hana budi kukifikia. Kila chembe ndogo, kila kitawi kidogo chanikiwiti, yeye anakiendea. Hana budi kukipata. Je, una kiu hivyo ya Mungu?

<sup>133</sup> Daudi alisema, “Hivyo ndivyo kiu ya—ya—yangu ilivyo, Mungu. Sina budi kuyapata, la sivyo nitaangamia. Nataka Uzima. Na fadhili Zako za upendo kwangu, ninapouhisi Uwepo Wako, nikiona maisha yangu yanaendana na Neno Lako, ni bora kwangu kuliko yote, kila kitu kingine, maisha mengine yote na kila kitu. Fadhili Zako za upendo!”

Ungama kosa lako sasa, tunapomba.

<sup>134</sup> Sasa, Bwana, umeiona hiyo mikono. Unawajua watu hao. Nami naomba ya kwamba utasamehe kila dhambi. Umba ndani yao kiu hii kuu inayokuja, wanayotamani. Mioyo yao ina njaa.

<sup>135</sup> Kila mtu ulimwenguni leo, ninawazia hii, nchi yetu, wazimu-wa anasa. Ee Mungu! Filamu, televisheni, maskini hadithi chafu! Na kusikia inahitaji madaktari watatu au wanne wa magonjwa ya akili kumweka Elvis Presley kwenye skrini, na Arthur Godfrey na wengi wa hao wengine. Ilifichuliwa tu juma lililopita, na mwandishi huyu wa habari wa New York, kwamba anawatembelea na wanawajua madaktari watatu au wanne wa akili, kwa kila mmoja, kujaribu kuushusha ulimwengu huu kufikia mahali pa mizaha miovu, michafu, mibaya, ya kuchukiza, isiyokaguliwa.

<sup>136</sup> Na—na wanawake mitaani, jinsi wanaume wanavyoingia wazimu, wakienda mahali mbalimbali; na kutengeneza nguo chafu za kujivika. Na tukitambua, Bwana, ya kwamba maskini binti huyo huko nje mitaani, huku akiuanika maskini mwili wake, na nguo zinazoonekana za kizinifu. Na mwanamume huyo kule kwenye baa, asubuhi ya leo, akijua ya kwamba anajaribu kuridhisha kiu aliyopewa na Mungu ya kumwonea Yeye kiu, kiu ya Mungu, anajaribu kuiridhisha kwa mambo ya kilimwengu, mambo ya ulimwengu. Tunaomba, Mungu, kwamba kwa njia moja au nyingine. . . Sijui vipi, lakini nadhani inabidi iwe ni saa hii.

<sup>137</sup> Lakini kwa wale walio na mwito, na wameinua mikono yao, wape, Bwana, kitu kile moyoni mwao wanachohitaji. Kiu hiyo iliyobarikiwa, na ikatishwe leo, kwa kufanywa upya kwa Roho Mtakatifu akizilowesha nafsi zao na kuwapa kile wanachotamani. Ninaomba katika Jina la Kristo. Amina.

Kuna Nchi iliyo ng'ambo ya mto,  
Tunayoiita hiyo tamu milele,  
Nasi tunafika tu kwenye ufuko huo kwa azimio  
la imani;  
Moja kwa moja tutafika langoni,  
Pale tukaishi pamoja na wasiopatikana na  
mauti,  
Watakapigwa hizo kengele za dhahabu kwa  
ajili yako . . .

Sasa uvumisheni, kwa urahisi sana sasa.

Hivi husikii hizo kengele sasa zikilia?  
Huwasikii Malaika wakiimba? (Hapo ndipo  
yote yanapoungana zikawa moja.)

Ile Yubile tukufu haleluya.  
Katika milele ile tamu iliyo mbali sana,  
Ng'ambo tu ya mto unaong'aa,

Watakapopiga kengele hizo za dhahabu kwa  
ajili yangu na yako.

<sup>138</sup> Ni wangapi wanaompenda? Inua mkono wako. Mshukuru Bwana. Sasa nyosha mkono moja kwa moja, peana mikono na mtu aliye karibu nawe, useme, “Mungu akubariki.”

. . . hizo kengele sasa zikilia?  
Huwasikii Malaika . . . (Hakika, sisi ni raia wa  
Ufalme.)

Hiyo ni Yubile ya utukufu haleluya.  
Katika milele hiyo tamu iliyo mbali sana,  
Ng’ambo tu ya mto unaong’aa,  
Watakapopiga kengele hizo za dhahabu kwa  
ajili yangu na yako.

<sup>139</sup> Sasa, Baba, pokea roho zetu na ibada zetu, tunapozikabidhi Kwako. Nasi tunajitayarisha tu kuwaombea watoto wagonjwa sasa. Tunaomba kwamba Roho Wako akae juu yetu. Ili tuweze kuomba maombi ya imani kwa ajili ya wale walio na haja saa hii. Tujalie, Baba. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

<sup>140</sup> Sasa naomba wagonjwa wakusanyike kuizunguka madhabahu huku tukiwapaka mafuta na kuomba pamoja nao. Tutafurahi kuwasaidia. Tutaimalizia ibada, mnaweza kukaa kwa dakika kumi, kumi na tano zijazo.

<sup>141</sup> Vema, tupe—tupe, Dada Gertie, “Kesho yenye furaha inaningojea.”

. . . nangojewa na kesho yenye furaha,  
Ambapo malango ya lulu yatafunguliwa wazi,  
Ndipo nitakapovuka pazia hili la huzuni,  
Nitapiga kambi kwenye Ng’ambo ya pili.

Siku moja mbali na ufahamu wa mwanadamu,  
Siku moja, Mungu ndiye tu anayejua ni wapi  
na ni lini,

Magurudumu ya uhai wa mwanadamu yote  
yatasimama kimya, (Itakuwaje basi?)

Ndipo nitakwenda kuishi juu ya mlima Sayuni.

Siku moja mbali na . . . (Wazia hilo!) . . .  
ufahamu wa mwanadamu

Siku moja, Mungu ndiye tu anayejua ni wapi  
na ni lini, (Itakuwaje?)

Magurudumu ya maisha ya kibinadamu yote  
yatasimama kimya,

Ndipo nitakwenda kuishi juu ya mlima Sayuni.

Pembea chini, ewe gari zuri,

Loo, linakuja kunibeba linipeleke Nyumbani;

Pembea chini, ewe gari zuri,

Linakuja kunibeba linipeleke Nyumbani.

Ni Meli ya Kale ya Sayuni,  
 Ni Meli ya Kale ya Sayuni, (Utukufu!)  
 Ni Meli ya Kale ya Sayuni,  
 Ipande, ipande.

Imemfikisha baba yangu mzee,  
 Imemfikisha baba yangu mzee,  
 Imemfikisha baba yangu mzee,  
 Ipande, ipande.

Ni Meli ya Kale ya Sayuni,  
 Ni Meli ya Kale ya Sayuni,  
 Ni Meli ya Kale ya Sayuni,  
 Ipande, ipande.

<sup>142</sup> Ndugu Craig, [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ndugu Junie, nyote njoni huku, mwombe pamoja na wagonjwa. Nyinyi wengine, Ndugu John, yeyote wenu anayetaka kuja, njoni moja kwa moja.

Loo—loo, si itakuwa [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] ni ajabu Kule,  
 Pasipo na mzigo wa kubeba?  
 Kuimba kwa furaha huku kengele za moyoni zikilia,

Loo, si itakuwa ni ajabu Kule?

Si itakuwa ni ajabu, (ajabu) kule,  
 Pasipo na mzigo wa kubeba?  
 Kuimba kwa furaha huku kengele za moyoni zikilia,

Loo, si itakuwa ni ajabu Kule?

Kutembea na kuzungumza na Kristo, aliye Mkuu,

Si itakuwa ni ajabu Kule?

Kutembea na kuimba pamoja na Kristo, aliye Mkuu,

Si itakuwa ni ajabu Kule?

Si itakuwa ni ajabu, (ajabu) Kule,  
 Pasipo na mzigo wa kubeba, (Huko)?  
 Kuimba kwa furaha huku kengele za moyoni zikilia,

Loo, si itakuwa ni ajabu Kule?

<sup>143</sup> Tunapoyawazia mambo hayo, ni kuu na ya ajabu vipi! Loo, Yeye ni halisi kwetu. Si itakuwa ni ajabu kule? Tabibu mkuu sasa yupo. Anataka kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka. Anataka kuwapa nguvu waliochoka. Anataka kuponya wanaoteseka.

<sup>144</sup> Sasa hebu na tuiname sasa katika Uwepo Wake tunapomtolea sifa zetu.

<sup>145</sup> Ee Tabibu Mkuu, mioyo yetu inapougua sana, tunalia kama kondoo Wako. Nasi tunasikia Roho Wako akirudi kwetu.

“Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu.” Nasi tunapenda kutangaza sifa Zako. Tunapenda kulia Mbele Zako kwa furaha. Tunapenda kukuelezea Wewe hisia zetu, kwa sababu tunakupenda kwa yote yaliyo ndani yetu. Nafsi yetu yote, akili, na mwili unampenda Bwana.

<sup>146</sup> Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba utatupatia hili, kwa kina zaidi na zaidi, daima. Jalia liwe halisi sana kwetu, hata ulimwengu utafifia, na upumbavu wake wote, ndipo hautawaziwa tena. Utafifia na kuingia katika Umilele. Ulikuwa na mwanzo, sasa na uwe na mwisho, pia. Tunajua utakuwa nao.

<sup>147</sup> Na sasa tunaomba, Mungu, wakati sisi, watoto Wako, tunaposimama hapa, tukiombeana mmoja na mwenzake, katika Jina la Bwana Yesu, kwa ajili ya udhaifu ulio katika miili yetu, uliosababishwa na dhambi za kale, na wa uovu wa ulimwengu, na miili yetu ipatikanayo na mauti. Imetiishwa sana na ya adui kwa sababu bado ni dhambi. Nasi tunasema kwamba Biblia inatutangazia, dhahiri, kwamba, “Roho Mtakatifu husaidia udhaifu wetu, na maombezi.”

<sup>148</sup> Nasi twaja Kwako, Baba, asubuhi ya leo, kwa unyenyekevu, tukiamini ya kwamba utatufanyia maombezi sasa, kwamba, tunapoungama dhambi zetu, na makosa yetu, na shauku zetu Kwako. Mioyo yetu ina njaa ya kuwa wazima, ili tuweze kutumika na kufanya kazi ambayo Wewe ungetaka tuifanye. Jalia, Bwana, wakati mzee Wako anaposonga mbele akiwapaka mafuta, nami naja nikiweka mikono juu ya wagonjwa, jalia Roho aje akiponya. Tunaomba haya yatimie, kwa njia ya Yesu Bwana wetu.

Sasa, mzee, kama utanzia hapa kisha uje moja kwa moja.

<sup>149</sup> Kila mtu katika maombi, sasa, tukiimba pole pole *Tabibu Mkuu*. Kila mtu akiimba kwa upole.

<sup>150</sup> [Ndugu Branham anawaomba wagonjwa, maneno yake mengi hayatambuliki—Mh.]...?..[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

<sup>151</sup> Sijakosea, huyu ni Dada Craig. [Dada Craig anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Ninaelewa hali yako, Dada Craig, kwamba unaumwa sana, ilibidi uondoke...?..[Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham.]...?..Sasa tazama. Huko nje kabisa katika majangwa hayo, umetaabika sana na mume wako hapa, kwa ajili ya Kristo. Kitu kile kile ambacho mumesimamia, Dada Craig, ndicho kitu pekee kinachoweza kukusaidia sasa. Na kama mtumishi wa Mungu, na tukijua ya kwamba tunakupenda wewe na Ndugu Craig hapa, sisi sote hapa kanisani. Na tunaithamini kazi yenu jangwani, miongoni mwa Wahindi. Na kwamba umekuja sasa, hii ndiyo hospitali asubuhi ya leo. Hapa ndipo Tabibu anaposimama, Yule mkuu. Na kufanya upasuaji huo, tutakupa ninii...?..Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili. Huenda akataka

kushuka na kumchukua. Usiwe na shaka lolote, Dada Craig! Kama tu...?...

<sup>152</sup> Vema, Ndugu Neville, nenda ukawatie mafuta.

<sup>153</sup> Mpendwa Baba wa Mbinguni, huyu hapa mke wa mhudumu...?...huko kwenye jangwa lenye joto. Wahindi hao waliishi na wakalisikia, wakijaribu kuwavuta Kwako. Naye amesimama hapa kwenye madhabahu hii ndogo leo. Ee Baba mwenye rehema, huku sisi, huku mikono yetu imewekwa juu yake, kama ishara, tukiamini kwamba Biblia bado ndiyo Mapenzi ya Mungu yasiyoweza kukosea. Tunaweka mikono juu yake. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...nyeupe kama theluji,  
Hakuna ila Damu yake Yesu;  
Nini kinachoweza kunifanya mzima tena?  
Hakuna ila Damu yake Yesu.

Loo, mtiririko ni wa thamani...

<sup>154</sup> [Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.]...?...Mungu akubariki, dada.

<sup>155</sup> Mke wa Ndugu George Colvins yuko katika Hospitali ya Wagonjwa ya Norton, huko Louisville, kwenu ninyi mnaowatembelea mkawaone. Na—na Bibi Colvin, aliyekuwa na kansa ya tumbo, mama mkwe wa—wake ana nafuu kidogo. Kwa hiyo, tunashukuru kwa ajili ya hilo.

<sup>156</sup> Sasa, kwenu tu ninyi watu ambao ni wagonjwa, na mliombewa, ningetaka kusema hili, neno dogo tu. Nasi tumechelewa kidogo tu, lakini jambo dogo tu.

<sup>157</sup> Kuhusu uponyaji wa Kiungu, loo, ni jambo la ajabu sana. Na ni rahisi sana ku—kulikaribia, kama ukichukua tu mtazamo sahihi kulihusu, unaona.

<sup>158</sup> Sasa, lile ono nililoona, na kulieleza kanisani hapa, kuhusu maji, (mnakumbuka hilo), na bwawa likiwa upande wa kushoto, nao mto ukirudi nyuma *huko*, kila sehemu yake ilifunuliwa pale pale Canada, kikamilifu kabisa. Nao Mto Saskatchewan unapitia mashariki badala ya magharibi, nayo maporomoko yalikuwa upande *huo* badala ya huo mwingine. Kaingia ndani, na ni baridi, upepo ukivuma na theluji ikianguka, katoka humo, nalo jua linawaka. Kaingia moja kwa moja mle ndani, kapata kisiki cha kale, kila kitu, kikamilifu tu kadiri kilivyoweza kuwa. Na kubadilika kabisa katika huduma yangu. Kweli kabisa.

<sup>159</sup> Bwana alifunua hapa, majuma machache yaliyopita, jambo la kufanya kwa ajili ya upambanuzi, na kadhalika, imeanza kuwa baraka kuu zaidi. Nasi tunaweza kuwaombea watu zaidi.

<sup>160</sup> Na sasa, jukwaani, baada ya hayo maono kwisha, tuliyaita maono na jukwa-...kwanza, kwanza kabisa. Halafu basi watu walipokuja, ilikuwa mara ya kwanza, mtaona hizo shuhuda sasa.

<sup>161</sup> Sasa, hii hapa sababu, papa hapa. Kama—kama hatungekuwa tumelelewa pamoja. Mnaona, sisi ni watoto tu hapa, pamoja, ambao tumelelewa pamoja, hiyo ndiyo sababu hamjui. . . Mnajua ya kwamba ninapenda kuwinda na kuvua samaki, na kadhalika, na hilo—hilo ndilo linaloliondoa.

<sup>162</sup> Ndugu Bill ni ndugu yenu tu, mnaona, kwamba mnanipenda nami nawapenda. Mnaona? Nawe unakuja hapa, na, vema, kama—kama ulitaka taa zako zitengenezwe usingejali kunipigia simu, nije nifanye hivyo, nijaribu. Na kama nisingeweza, ningemwita Ndugu Rhody. Hivyo basi sisi tunaninii tu. . . ama kitu fulani, mwajua, kwa utaratibu huo. Mnaona? Na hiyo ni kawaida tu kati yenu. Mahali pengine inaonekana kuwa tofauti. Wakati sisi. . . Vema, sasa sisi. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hiyo ni mojawapo ya vipodozi, kama tu vile macho ya kahawia na ya bluu. Unaona, ni—ni moja tu ya vipodozi. Hatuwezi kuliepuka hilo.

<sup>163</sup> Huko Canada, nilipofika huko, vema, bila shaka, nimewaambia kilichotokea. Tulikuwa na maelfu kadhaa ya watu huko nje, lakini wengi wao walikuwa ni Waanglikana na Wabaptisti, na kadhalika, ambao walikuwa wameufadhili mkutano wangu. Wapentekoste ambao wamenikataa kabisa. Kwa hivyo, basi, ila hilo ni sawa, hilo. Nawapenda vivyo hivyo tu. Mnaona?

<sup>164</sup> Lakini mle ndani, usiku huo, mwanamke alikuja jukwaani, wa kwanza, mkutanoni. Naye alikuwa kipofu, sijui kwa muda gani. Kama vile tu yule mama anayekuja hapa tuliyemwombea. Ilibidi wamwongoze jukwaani, asingeweza kutofautisha mchana na usiku. Alikuwa hivyo kwa miaka mingi. Nami nikisimama pale, nikimwombea mwanamke huyo, macho yake yakafunguliwa jukwaani. Ndipo anashuka na kuchukua taipureta na kuniandikia ushuhuda wake mwenyewe.

<sup>165</sup> Aliyefuata, alikuwa mvulana mdogo ambaye alikuwa kabisa. . . Maskini huyu msichana hapa, alikuja hapa na kuomba muda mfupi uliopita, kuhusu mtoto mdogo aliyekuwa bubu. Tulikuwa na mtoto huyo pale jukwaani, nafikiri alikuwa yapata, loo, ningesema, umri wa miaka minane ama kumi. Hakuweza, hakujuu neno moja. Asingeweza kutamka chochote. Asingeweza kusikia kitu; hakuweza kamwe. Alizaliwa hivyo, hawezi kabisa kusikia, hawezi kuzungumza. Akasimama pale na kulia na kumsifu Bwana, naye aliweza kusikia chochote, na kukimbia jukwaani, akishangilia.

<sup>166</sup> Aliyefuata akaja, alikuwa ni mtoto mwenye kifafa, yapata umri wa miaka kumi na miwili. Billy alisaidia kumbeba jukwaani, pamoja na watu wawili. Alikuwa katika hali mbaya sana, namna *hii* tu, mnaona. Inanikumbusha juu ya maskini Edith Wright. Basi wakakileta maskini kitoto hicho pale. Basi nilipokuwa nikiomba, alisema, “Niwekeni chini. Yesu



ameniponya.” Vema, tungefanya nini ila kumweka chini? Basi, alipofanya hivyo, alitembea kupitia pale, akifanya *hivi*, [Ndugu Branham anapiga makofi—Mh.] akimsifu Mungu na kupiga makelele, na kutembea huku na huku mahali hapo namna hiyo. Na huku watu wanazimia, karibu wazimie, katika kusanyiko, namna hiyo.

<sup>167</sup> Kisha akaja maskini kibyongo, nundu kubwa mgongoni mwake. Naye alikuwa Mkatoliki. Bila shaka, tunaelewa, wanaamini katika uponyaji. Sasa, kwenu ninyi Wakatoliki, sina neno dhidi yenu. Hilo ni sawa, mnaona. Bali wanaamini vitu kama sanamu, na kadhalika, mnaona. Ndipo—ndipo nikasema, “Sasa angalia, mwanangu, hatuamini katika uponyaji kwa njia hiyo. Hatuamini katika kugusa sanamu. Tunaamini ya kwamba sisi, kwa neema ya Mungu, ni wana na binti za Mungu, unaona, na Roho wa Mungu yuko ndani yetu.”

<sup>168</sup> Nami nikasema, “Sasa hivi ndivyo tunavyoamini. Huyu hapa anakuja. . . Yesu alipitia hapo, siku moja, na kulikuwako na mti umesimama pale. Naye akasema. . . Alitafuta tunda, wala hapakuwapo na tunda, ndipo akasema, ‘Hakuna mtu atakayekula kutoka kwako, tangu. . . hata milele,’ akaendelea mbele. Basi kesho yake, walipopitia hapo, mti huo ulikuwa umenyauka. Petro akasema. . . Mbona, mnamjua Petro—Petro, jinsi alivyokuwa. A—akasema, ‘Mbona, uangalieni ule mti! Uangalieni.’ Naye Yesu akasema, ‘Mwaminini Mungu. Kwa maana ukiuambia mlima huu, “Ng’oka,” wala usione shaka, bali uamini kwamba hayo uyasemayo yatatimia, yatakuwa yako.” Nikasema, “Unalipata hilo?”

“Naam.”

<sup>169</sup> “Mnaposali, aminini kwamba mnapokea kile mwombacho, kitakuwa chenu.”

<sup>170</sup> Nikasema, “Unaona, sisi, baada ya kumpokea Roho wa Mungu. . . Sasa, Mungu aliumba ulimwengu kutoka kwa utupu. Ni Neno Lake tu. Aliumba tu. Neno Lake ni umbaji. Kwa hiyo, Yeye alinena tu, nao ulimwengu ukaumbwa. Kwa sababu, Hilo lilikuwa ni madhumuni niani mwa Mungu, moyoni Mwake. Alilinenena tu, nalo likawa. Alikuwa Muumba.” Nikasema, “Basi, kama tuna *Zoe*, Uhai wa Mungu ndani yetu, tunakuwa wana wa Mungu, na waumbaji wadogo,” Nikasema, “maana Yeye alisema, ‘Lolote usemalo, amini kwamba hayo uliyosema, yatakuwa yako.’”

<sup>171</sup> Nami nimeona hilo. Mara nyingi, ningesema mambo ambayo ilikuwa vigumu kwangu mwenyewe kuyawazia, lakini ningeyasema, kwa vyovyote vile. Ndipo nikaja kugundua, yalitimia vivyo hivyo tu. Ningesema mambo ambayo sikukusudia yatokee hivyo, lakini yalitokea, kwa vyovyote vile, kwa sababu nilikuwa nimeyasema. Nikawazia, “Ngoja kidogo!”

172 Kwa hiyo, nikasema, “Unaona, tunapozungumza chochote, kama jambo fulani limetia nanga kwetu, kamwe hatupaswi kulizungumza mpaka tuliamini. Ndipo tunapoliamini, tunalinena, ndipo Neno hilo la uumbaji linatokea. Ni sehemu ya Mungu, unaona, Nalo liliumba.”

173 Kasema, “Naelewa.” Nikamkumbatia, nikamwombea.

174 Nikijua kuwa yeye ni Mkatoliki, nilisema, “Sasa, wewe ngoja tu. Usiku wa leo, utakapoenda nyumbani, jizungushie kamba ndogo, namna *hii*, na kuikaza. Acha mama afanye hivyo. Kisha ikate. Halafu, kesho usiku, kama haijapungua inchi tatu, basi mimi ni nabii wa uongo. Irudishe, na ulete kamba iyo hiyo. Ikate, kisha uiweke hapa.”

175 Baada ya yeye kuondoka, niliwazia, “Nilisema nini? Nilisema nini? Vipi kama huo ungalikuwa ni ukosoaji fulani pale, mnaona?” Nikawazia, “Lakini, kama Mungu alisema hilo, maana sikujua ningelisema, kwa hiyo nitaliacha tu namna hiyo.” Mwache aendeleo mbele.

Kesho yake usiku, ilikuwa tu karibu ndefu *hivyo*, angalieni mahali ilipo.

176 Kwa hiyo, aliyefuata, wachache baada ya huyo, alikuwa ni mvulana mdogo aliyepita, nundu ndogo mgongoni mwake, imetokeza namna *hiyo*. Kulikuwa na kundi zima la Wakatoliki wa Canada wa Kifaransa waliokuwa wameshuka huko, nao wakaokoka na kujazwa na Roho Mtakatifu pale. Mnaona? Naye maskini mvulana huyu alikuwa na mkono, umeshuka namna *hiyo*, nundu ndogo mgongoni mwake. Jamaa mdogo sana, karibu namna *hii*, akapita. Nami nilikuwa nikitaka kumwombea. Nikasema, “Mpenzi, unaona nilichomwambia yule mvulana mwingine kuhusu maskini bega lake?” Ndipo, basi, unaona, maskini hao vibyongo, hawawezi kuinua mikono yao namna *hiyo*. Mnaona, wamebanwa, kitu fulani kinaingia mgongoni mwao hapa.

177 Akasema, “Naam, bwana.” Kasema, “Siwezi kurudi.” Nikaja kutambua, yeye alikuwa wa familia maskini sana, huko mbali British Columbia. Mnaona? Hakuwa na pesa, kukaa muda mrefu zaidi.

178 Nikasema, “Vema, Mungu atakuponya, mpenzi.” Nikamkumbatia.

179 Sasa, si—si—si—sitaki ku—kusema jambo lisilo kweli. Ni—ni—ninataka kusema yaliyo kweli, mnaona. Basi nilikuwa nimemkumbatia huyo jamaa mdogo, huku mkono wangu ukiwa juu ya nundu hiyo kubwa. Nami nikahisi kama nundu hiyo imesogea na mkono wangu ukashuka chini.

180 Kwa hiyo, nilipoacha kuomba, nilimtaazama. Maskini macho yake madogo yakametameta. Nikasema, “Unahisi hilo?”

Akasema, “Naam, bwana, nilihisi.”

181 Nami nikatazama pande zote, hapakuwa na nundu yoyote pale. Nikasema, “Inua mkono wako.” Na huyu hapa akaenda, mzima kabisa, moja kwa moja mbele ya wasikilizaji pale.

182 Na, loo, hiyo ilikuwa ni ninii tu...Loo, sijui ni mambo mangapi makuu aliyofanya Bwana wetu, kila usiku, ya viziwi, mabubu, vipofu.

183 Nanyi mnamjua yule msichana mdogo ninayewaambia habari zake, huko Ujerumani, aliyekuwa na yale...Mnajua jinsi alivyopanda jukwaani, jambo lililowafanya wakomunisti... kuwanyamazisha...kuwanyamazisha kabisa? Hadithi hiyo ilijirudia kikamilifu. Msichana mdogo alikuja, alikuwa na misokoto mirefu, maskini uso uliochongoka; kipofu, wakamwongoza kupanda juu. Nami nikasema, “Anaonekana kama yule msichana mdogo wa Kijerumani; macho madogo meupe.” Nikasema, “Anaonekana kama yule msichana mdogo wa Kijerumani ambaye alikuwa huko Ujerumani.” Nikasema, “Ni wangapi hapa ndani waliowahi kusoma ama kusikia kwenye kanda, na kadhalika.” Na, loo, mamia na mamia ya mikono. Nikasema, “Anaonekana tu kama yule msichana mdogo Mjerumani.” Nami nikasema, “Wewe ni baba yake?”

Akasema, “Naam, bwana.”

Nikasema, “Uraia wake ni upi?”

184 Kasema, “Mimi ni Mjerumani.” Kasema, “Sisi ni—sisi ni Wajerumani.” Yeye na mke wake, wote wawili.

185 Vema, yule msichana mdogo Mjerumani, hasa, hiyo misokoto midogo ikining’inia mgongoni mwake namna hiyo. “Loo,” nikawazia, “Bwana, laiti ungefanya hivyo tena!” Mnaona? Sasa ni nini? Nikawazia, “Sasa, kama naweza tu...Nipewe imani hiyo, kujua kwamba itakuwa hivyo, ninaweza kulinena, nami ninaamini litatendeka.” Lakini, kwanza, haina budi kutendeka hapa kwanza. Mnaona?

186 Kwa hiyo nikaipata, pamoja na huruma yote niliyoweza kwa mtoto huyo mdogo, nami nikamwinua hivyo. Ndipo nikasema, “Je, unaweza kuona chochote?”

“La, bwana.”

187 Kasema, “Hajaona.” Loo, sidhani yeye...Labda hajawahi kuona. Sijui tu ni muda gani umepita tangu alipoona; na labda kamwe hajapata kuona. Macho yake madogo, kama tu mipira midogo myeupe juu yake, namna hiyo.

188 Na kwa hiyo nikamshikilia huyo mtoto mdogo namna *hiyo*, na kumwomba. Naye alikuwa akitabasamu nilipomwachilia. Nikasema, “Unaona, mpenzi?”

189 Kasema, “Ndiyo, bwana.” Naye akaanza kutabasamu, machozi madogo yakitiririka kwenye mashavu yake madogo. Mtoto mdogo tu, namna *hiyo*.

Nikasema, “Unaona kweli?”

Akasema, “Naam, bwana.”

<sup>190</sup> Nikasema, “Sasa njoo hapa nilipo, na uweke kidole chako kwenye pua yangu.” Naye huyu hapa akaja, akitabasamu namna hiyo, akaenda na kuweka kidole chake kwenye pua yangu.

Nikasema, “Nimeinua vidole vingapi?”

<sup>191</sup> Akasema, “Una vitano.” Ndipo baba yake nusura azimie.

Nikasema, “Ulisema nini kipenzi? Vidole vingapi?”

<sup>192</sup> Akasema, “Una kimoja tu sasa.” Naye huyo hapo, kipofu kabisa, akafumbuliwa macho yake.

Loo, Yeye ni wa ajabu! Ka—karibu haliaminiki.

<sup>193</sup> Lakini, marafiki, huenda nikarudi usiku wa leo. Kama sivyo, labda Jumapili ijayo. Msisahau mkutano wetu huko Indianapolis, kuanzia sasa.

<sup>194</sup> Tazama, nina jambo ninalotaka kuongea na kanisa. Ni ujumbe juu ya nyakati. Tuko mwisho, jamani. Angalieni, angalieni tufani hizi na vimbunga hivi. Havijawahi kusikika. Angalieni matetemeko ya nchi, kila kitu, kila taifa. Isitoshe, ndugu, wanazungumza kuhusu mpango huu wa upunguzaji wa silaha. Hivyo ndivyo hasa ibilisi anavyotaka. Kuzilundika tu huku, kusudi tuweze kulipua kitu hicho chote. Hivyo ndivyo anavyotaka hasa. Mnaona? Loo, tunaishi juu ya kipipa cha baruti, nayo fyuzi iko mwishoni.

<sup>195</sup> Yale niliyozungumzia, asubuhi ya leo, *Uzima*, loo, utafuteni huo kwa moyo wenu wote. Nisingeweza. . .

<sup>196</sup> Ukiwaambia watu mambo mengi kupita kiasi, wanachanganyikiwa kabisa wala hawajui unalosema basi, unaona. Ni. . .Huwezi kuzungumza na watu. . .Jambo moja tu kwa wakati mmoja, ndiyo njia bora ya kulipata. Wala sina ninii tu. . .Labda mkutano mmoja, mara kwa mara, pamoja nanyi, wala siwezi kuwaambia jinsi ninavyotaka, mnaona. Nanyi mnachanganyikiwa kabisa ninapoanza kuwaambia mambo mengi kupita kiasi.

<sup>197</sup> Lakini jambo hili moja kumbukeni, asubuhi ya leo, utafuteni *Uzima*. Loo, utafuteni. Uoneeni kiu. Endeeleni tu kuufikia. Msiruhusu chochote kiwazuie. Utafuteni.

Na mpaka tutakapofanya hivyo, tunapoondoka, inatubidi kufanya nini?

Peleka Jina la Yesu,  
Tukisujudu miguuni Pake,  
Tutamvika taji kama Mfalme wa wafalme,  
Mbinguni,  
Safari yetu itakapokamilika.

Vema, tusimame kwa miguu yetu.

Peleka Jina la Yesu,  
Mtoto wa huzuni na majonzi;  
Litakupa furaha na faraja,

<sup>198</sup> Nitawaambia tufanye nini. Geuka moja kwa moja na kupeana mikono na mtu hapo, ukisema, “U hali gani, ndugu? Hakika nina furaha kufahamiana nawe.”

Jina la Thamani, (Loo jinsi lilivyo tamu!)  
. . . na furaha ya Mbinguni;  
Jina la Thamani, (Jina la Thamani!) Loo jinsi  
lilivyo tamu!  
Tumaini la duniani na furaha . . .

<sup>199</sup> Sasa angalieni huku tena. Tuna furaha kuwa pamoja nasi asubuhi ya leo, Ndugu George Craig kutoka Arizona, mmoja wa ndugu zetu. Tuna furaha kuwa na Ndugu Whitney hapa, kutoka St. Louis. Atakuwa kwa Ndugu Cauble usiku wa leo, katika fundisho la unabii, kutoka kwenye chati, kwenye kanisa la Ndugu Cauble. Ha—halafu Ndugu Junior Jackson yuko kule nyuma, na pia Ndugu—Ndugu Collins, na Ndugu John O’Bannon, na—na wahudumu wengine wengi hapa. Sote tuna furaha kuwaona humu sasa.

Tukiliinamia Jina la Yesu,  
Tukisujudu miguuni Pake,  
Tutamvika taji kama Mfalme wa wafalme  
Mbinguni,  
Safari yetu itakapokamilika.

Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu!  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;  
Jina la thamani, Loo jinsi lilivyo tamu! (Loo  
jinsi lilivyo tamu!)  
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni. 🐦

57-0602 Uhai  
Branham Tabernacle  
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)